Global Schools Program

# MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU




# Muhtasari wa kozi

## Darasa la 10

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Kuwawezesha wanafunzi kuboresha ulimwengu katika masomo sitini*. 1st ed. Createspace Independent Publishing Platform.

**Hati Miliki:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Kutazama nakala ya leseni hii tembelea, https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa na kuchapishwa kwa kujitegemea na Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo la Kujifunza**<br>Mtaala wa Darasa la 10 unaangazia umuhimu wa mwanafunzi kipekee. Katika kipindi cha somo, wanafunzi watatambua maadili yao wenyewe, kuchunguza jinsi wanavyoyaeleza maadili yao kupitia matendo yao na pia wataenda kwenye jumuiya zao kuona jinsi gani wanaweza kuchangia katika kutatua matatizo ya ulimwengu halisi. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo la 1** | Mimi Binafsi |
| **Somo la 2** | Jumuiya yangu |
| **Somo la 3** | Kusawazisha sauti katika masuala ya kimataifa |
| **Somo la 4** | Dunia yetu |
| **Somo la 5** | Mradi wa msingi |
| **Malengo ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watatafakari kwa kina namna maadili yanavyohusiana na vitendo na kufanya mazoezi jinsi ya kukuza maadili yao katika hali ya kawaida.<br>• Wanafunzi watajihusisha na tatizo la ulimwengu halisi katika jumuiya yao wenyewe, wakizungumza na watu na kutengeneza suluhisho lao wenyewe.<br>• Wanafunzi watafanya mazoezi ya uandishi rasmi katika karatasi zao za mwisho. | |

**Darasa la 10 Somo la 1**
"Mimi Binafsi"

**Muda:** Dakika 60
**Somo:** Sanaa
**Viwango:** Kukomesha Umasikini (SDG 1); Kukomesha Njaa (SDG 2); Afya Bora na Ustawi (SDG 3); Elimu bora (SDG 4); Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (SDG 5); Kupunguza Kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (SDG 16); Ushirikiano kwa Malengo (SDG 17).
**Imeandaliwa na:** Sharon Jiae Lee

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, wanafunzi wataangalia maadili yao binafsi na kushirikishana darasani huku wakijaribu kujadili hali/mahali/matukio katika jamii na ulimwengu ambapo hayo maadili yanafuatwa na mahali hayo maadili hayapo. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuthamini msaada wa familia kwa kiwango cha juu na kupitia majadiliano atambue kwamba sehemu ambazo usaidizi wa familia unapokosekana zaidi ni vituo vya watoto yatima. Katika masomo yafuatayo, wanafunzi wataangalia kwenye jamii, taifa, na ulimwengu kutafuta suluhu kwa matatizo waliyoyabainisha, na hatimaye, kuorodhesha/taja matatizo na kutoa suluhu kwa matatizo wanayohisi kuwa na shauku kubwa kuyatatua katika karatasi

**Lengo la ufundishaji:**

- Wanafunzi wataweza kujijua vizuri zaidi kwa kutafakari juu ya maadili yao.
- Wanafunzi watajifunza kuwa na mijadala yenye tija juu ya maadili tofauti ya wanafunzi wengine na wajifunze kuheshimu tofauti hizo.
- Wanafunzi wataweza kutambua upungufu/matatizo katika jumuiya, nchi na/au ulimwengu wao pale ambapo maadili hayo yanapokosekana.

**Kuelewa malengo:**

- Watu wana maadili tofauti na hutenda kulingana na maadili hayo katika kufanya maamuzi ya kila siku.
- Maadili tofauti yanapaswa kuheshimiwa, na kama baadhi yao wanaonekana kutopatana, wanafunzi wanapaswa kuwa na uwezo wa kufanya midahalo yenye kujenga ili kuelewa na kutatua migogoro.

**Maswali Muhimu:**

- Maadili ni nini?
- Ni kanuni gani muhimu zaidi maishani?
- Kwa nini tunapaswa kujali kuhusu maadili?
- Ni wapi katika jumuiya, taifa, na/au ulimwengu wetu ambapo tunaona watu wakiyaishi/kutoyaishi maadili yetu?

**Malengo ya kujifunza ya mwanafunzi (Wanafunzi watatweza...): Tathmini**

| Lengo | Masharti | Ujuzi unaoonekana/ Kitabia | Tathmini |
|---|---|---|---|
| Kujifunza maadili na umuhimu wake | Darasani kwa ujumla | Wanafunzi watafahamu maadili ni nini na kwanini ni muhimu. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maadili ni nini na kwanini ni muhimu? |
| Kutafakari na kutambua maadili kibinafsi | Kazi binafsi | Wanafunzi watatambua thamani moja muhimu katika maisha yao. | Je, mwanafunzi anaweza kutambua thamani moja muhimu katika maisha yake? |
| kushirikiana na wanafunzi wengine kwenye vikundi | Kazi za vikundi | Wanafunzi watajadili kuhusu maadili yao wenyewe, watasikiliza kutoka kwa wengine, na watatoa maoni ya kujenga na watauliza maswali ya usaidizi. | Je, mwanafunzi anaweza kushiriki kwenye kikundi ?<br><br>Je, mwanafunzi ana heshimu maadili tofauti ya wanafunzi wengine<br><br>Je, mwanafunzi anaweza kuchangia maoni ya kujenga na/au kuuliza maswali muhimu? |
| Kuunganisha maadili ya wanafunzi kibinafsi kwa ulimwengu | Kazi ya kikundi | Wanafunzi watatambua matatizo katika jamii/taifa/ ulimwengu yanayokiuka maadili. | Mwanafunzi anaweza kufanya uhusiano kati ya maadili binafsi na jamii/ taifa/ulimwengu? |

**Mtiririko wa Shughuli:**

| Muda | Shughuli | Maswali |
|---|---|---|
| Utangulizi (dakika 20) | Mpatie kila mwanafunzi kipande cha karatasi. Fungua somo kwa kuuliza maswali yalio kwenye safu ya kulia.<br><br>Baada ya wanafunzi kadhaa kujibu maswali, waambie watafakari juu ya maadiili yao na wachore maadili moja la kimaadili. Wanapaswa kuchora tukio/ kitu ambacho kinawakilisha vyema maadili hayo. | Maadili ni nini? Kwa nini ni muhimu? |
| Uwasilishaji /Majadiliano ya kikundi (dakika 20)ujadili | Wanafunzi wagawanywe katika vikundi vidogo (vikundi viwe vidogo vidogo ili kila mwanafunzi apate nafasi ya kuwasilisha maadili yake.<br><br>Waambie/waulize wakisie maadili ya kila mmoja.<br><br>Wanafunzi watataja maadili yao, baada ya hapo waulize swali lililopo kwenye safu ya kulia.<br><br>Wanafunzi kwa pamoja wajadili maswali kwenye vikundi vyao. | Je, unadhani kila mmoja ni muadilifu? Kwa nini au kwa nini sivyo?<br><br>Je, ni sawa kuwa na maadili tofauti?<br><br>Je, maadili yote yanapaswa kupewa nafasi sawa?<br><br>Je, kama maadili yanakinzana/hayaendani na maadili yetu tunapaswa kufanyaje? |
| Majadiliano ya Kikundi (Dakika 15) | Waulize wanafunzi kuhusu maadili katika jamii/taifa/ dunia, kisha uliza maswali kwenye safu ya kulia. Wanafunzi wajadili wakiwa kwenye vikundi. | Ni wapi katika jamii yetu huwa maadili yako yanafuatwa ?<br><br>Ni wapi hapa nchini huwa maadili yako yanafuatwa ?<br><br>Ni wapi duniani huwa maadili yako yanafuatwa ? |
| Kufunga/Hitimisho (Dakika 5) | Wakaribishe baadhi ya wanafunzi wajitolee kuwasilisha michoro yao na maadili yao darasani. Uliza swali lililopo kwenye safu ya kulia. Wahimize wanafunzi wawe wafanya mabadiliko katika jamii zao na duniani. | Tunatakiwa kuchukua hatua zipi tunapoona matatizo duniani yanayoenda kinyume na yale tunayo chukulia kuwa ya muhimu maishani? |

**Nyenzo kwa  Wanafunzi**

- Wewe na maadili yako: https://www.goodcharacter.com/middle_school/you-and-your-values/
- Chaguzi na Maadili: https://www.nwabr.org/sites/default/files/ValuesActivities.pdf

**Zana za walimu**

- https://www.uen.org/lessonplan/view/562
- https://www.educationworld.com/a_lesson/lesson/lesson329.shtml
- https://sustainablelifestyleseducation.org/theme/values-ethics/
- http://cup.columbia.edu/book/ethics-in-action-for-sustainable-development/9780231202879

**Darasa la 10 Somo la 2**
"Jumuiya yangu"

**Muda wa muafaka:** Dakika 60
**Masomo:** Masomo ya Jamii
**Viwango:** Kukomesha Umaskini (SDG 1); Kukomesha Njaa (SDG 2); Afya Bora na Ustawi (SDG 3); Elimu Bora (SDG 4); Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (SDG 5); Kupunguza Kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (SDG 16); Ushirikiano kwa Malengo (SDG 17)
**Iliyoundwa na**: Quinn Lockwood

**Muhtasari na Mantiki:** Wanafunzi wataendeleza somo la kwanza ambalo walijadili juu ya maadili yao na kuandika matatizo yanayoikabili dunia ambayo wana shauku ya kuyatatua. Katika somo hili, wanafunzi watajiandaa kwenda katika jumuiya yao ya karibu na kufanya mahojiano na watu binafsi au pengine watu kadhaa ambao ni wanachama wa shirika linalojishughulisha na shughuli za kutatua matatizo walioyoyabaini. Hii inaweza kufafanuliwa kwa upana (kwa mfano, kunaweza kusiwe na mtu katika jumuiya ya eneo hilo anayefanya kazi inayoshughulikia suala/tatizo halisi la mwanafunzi).

**Malengo ya mafundisho:**

- Mwalimu atawaongoza wanafunzi katika kuoanisha tatizo walilolitambua na mtu /shirika katika jumuiya yao ambaye/ambalo anajihusisha na jitihada za kushughulikia tatazo hilo.
- Mwalimu atawasaidia wanafunzi kuunda utaratibu wao wa usaili na kuhakikisha wanafunzi wanaweza kufanya mazoezi ya kuwa wahojaji (kwa kushirikiana na wanafunzi wenzao kama wahojiwa).
- Mwalimu anaweza kujadili masuala kama vile kurekodi mahojiano, ili kupata maana ya taarifa wanazopata kutoka kwenye mahojiano, na jinsi ya kujumuisha mahojiano kwenye karatasi yao ya mwisho.

**Kuelewa Malengo:**

- Kuelewa Elewa umuhimu wa kuzungumza na watu kuhusu kazi wanayofanya.
- Kuelewa Elewa jinsi ya kuundaa maswali ya kuuliza katika mahojiano.
- Kuelewa Elewa jinsi ya kufanya ulinganifu kati ya kazi ambayo watu hufanya katika ngazi ya mtaa na jinsi kazi hii inavyoweza kuathiri masuala ya kijamii.
- Kutambua Elewa njia ambazo fasihi zinaweza kuwakilisha kwa usahihi na kwa njia isiyo sahihi na hali halisi ya kijamii na kitamaduni.

**Maswali Muhimu:**

- Kusudi la kufanya mahojiano ni nini?
- Ni njia ipi bora ya kuwasiliana na watu na kuwaeleza kile ambacho tungependa kuzungumza nao ?
- Je, tunawezaje kufikiria maswali ambayo yanajibu yale tunayotaka kujua kuhusu matatizo tuliobaini hapo awali?
- Tunaweza kutumiaje vizuri habari tunazopata kutokana na mahojiano?
- Tunawezaje kuhakikisha kwamba tunaheshimu muda wa wenzetu katika hili zoezi?
- Ni changamoto zipi zinazoweza kutokea wakati wa mahojiano yetu?
- Je, ni baadhi ya mikakati gani tunaweza kufikiria ili kushughulikia changamoto hizo?

**Malengo ya mwanafunzi ya Kujifunza Malengo ya Somo (Wanafunzi wataweza):**

- Kutengeneza maswali ya mahojiano.
- Kufanya mazoezi ya mahojiano.
- Kuandaa muhtasari wa walichogundua katika mahojiano ya majaribio.
- Kuundaa orodha ya maswali watakayouliza kwenye mahojiano yao na wanajumuiya.

**Tathmini:** Wanafunzi watakamilisha mahojiano ya majaribio na wanafunzi wenzao, pamoja na kuunda orodha ya maswali ya mahojiano na uandishi mfupi wa matokeo yao kutokana na mahojiano. Wanafunzi watawasilisha utaratibu wao wa usaili na maswali kwa ajili ya mwalimu kuyapitia kabla ya kwenda kwenye jumuiya kufanya mahojiano.

**Mlolongo wa Shughuli:**

**Maandalizi ya Mwalimu:** Kabla ya somo, mwalimu anapaswa:

- Kuchagua wanajumuiya ambao watahojiwa na wanafunzi kulingana matatizo waliobainisha katika darasa lao la mwisho.
- Wanafunzi watahitaji kufanya utafiti wa awali kuhusu mada yao kabla ya kubuni maswali ya mahojiano. Wajulishe wanafunzi mshirika wao wa jumuiya watakaomhoji ni nani kabla ya somo hili.
- Wape wanafunzi kazi ya utafiti ya kukamilisha kabla ya darasa hili ambayo itawawezesha kuwa na uelewa wa kimsingi wa kile ambacho washirika wao wa jumuiya hufanya kabla ya kuandaa maswali ya mahojiano.

**Tambulisha Mada (dakika 5):**

- Pangilia somo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa watakuwa wakifanya mazoezi ya ujuzi wa kuhoji, pamoja na kupata nafasi ya kujiweka katika nafasi ya mhojiwa.
- Wakumbushe wanafunzi kwamba katika darasa la mwisho, walichunguza suala la maadili na wakatumia maadili yao kubaini matatizo yaliyomo katika jamii yao.
- Wajulishe wanafunzi kuwa wewe (mwalimu) umewatambua baadhi ya washirika, iwe ni mashirika au watu binafsi, ambao wanafanya kazi ya kushughulikia masuala ambayo wanafunzi waliibua wakati wa darasa la mwisho. Wanafunzi wataweza kuwahoji wanajamii hawa na kutumia taarifa katika mtihani wao wa mwisho. Ili kufanya mazoezi kwa mahojiano haya, wajulishe wanafunzi watakuwa wakifanya mazoezi ya kuwahoji wanafunzi wenzao.

**Kujitayarisha (Dakika 20):** Anzisha mazoezi ya haraka ya usaili kwa wanafunzi. Waweka wanafunzi katika vikundi vya watu wanne, na acha jozi moja ianze huku jozi nyingine ikitazama, kisha wabadilishane. Toa kwa kila jozi ya wanafunzi orodha ya sampuli ya maswali ya usaili (hapa chini katika "Nyenzo za Walimu") na ipe kila jozi dakika 10 kuhojiana (kila mwanafunzi katika kila jozi hupata dakika 5).

**Tafakari (Dakika 5):** Wape wanafunzi fursa ya kuzungumza katika kundi lao la wanafunzi wanne kuhusu nini kilikwenda vizuri na nini kingekuwa bora wakati wa mahojiano ya mazoezi. Toa maswali elekezi kwa wanafunzi, kama vile:

- Ulijisikiaje ulipokuwa ukiuliza maswali?
- Je, ni baadhi ya mambo gani yenye changamoto uliyokumbana nayo ukiwa mhojaji ?
- Je, ni baadhi ya mambo gani yenye changamoto uliyokumbana nayo ukiwa mhojiwa?

**Kujenga Maswali na taratibu za Mahojiano (dakika 10):** Sambaza kitabu (hapa chini katika "Nyenzo za Walimu") chenye vidokezo na mbinu bora za usaili. Pitia kitabu na wanafunzi baadaye wape nafasi ya kushirikishana mawazo yao kuhusu jinsi ya kutumia mazoea haya wakati wa kuendeleza maswali yao ya mahojiano.

**Mazoezi ya Mahojiano (dakika 10):**

- Mpe kila mwanafunzi kazi/tatizo lake na uwape jukumu la mtu/shirika linalofanya kazi kushughulikia tatizo hilo.
- Wape kila jozi ya wanafunzi sampuli chache za maswali kisha uwape dakika tano za kuunda baadhi ya maswali ya sampuli kwa kujitegemea.

- Baada ya dakika 5 za kupanga, wape wanafunzi dakika 5 kufanya mazoezi ya kuuliza na kujibu maswali.

**Kushirikiana Darasani (dakika 10):**

- Wape wanafunzi nafasi ya kuwasilisha maswali yao na kupokea maoni kutoka mwalimu na wanafunzi wenzao. Kama kazi ya nyumbani, wanafunzi wanapaswa kupanua orodha yao ya maswali na kuhariri maswali yao kulingana na maoni waliyopokea.
- Wanafunzi watakuwa na jukumu la kuwasiliana na washirika wao wa jumuiya ili kupanga mahojiano, kwa msaada kutoka kwa mwalimu kama inahitajika. Wajulishe wanafunzi iwapo wana fursa ya kupanga mahojiano ya simu ikiwa mahojiano ya ana kwa ana hayawezekani.

**Zana za Walimu:**

- Maswali zaidi. Kujifunza Sanaa ya Mahojiano: https://archive.nytimes.com/learning.blogs.nytimes.com/2010/09/20/beyond-question-learning-the-art-of-the-interview/?_r=1

**Darasa la 10 Somo la 3**

"Kusawazisha Sauti katika Masuala ya Ulimwenguni"

**Muda muafaka:** dakika 60
**Masomo:** Jiografia, Somo la Jamii
**Viwango:** Kukomesha Njaa (SDG 2); Afya Bora na Ustawi (SDG 3); Elimu bora (SDG 4); Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (SDG 5); Maji Safi na Usafi wa Mazingira (SDG 6); Viwanda, Ubunifu na Miundombinu (SDG 9); Miji Endelevu na Jumuiya (SDG 11); Maisha Chini ya Maji (SDG 14); Maisha kwenye Ardhi (SDG 15)
**Imeandaliwa na:** Holing Yip

**Muhtasari na Mantiki:** Katika kuchanganua matukio ya kimataifa, ni muhimu kutambua kwamba maoni juu ya masuala hutegemea sana mtazamo ambao unakagua suala hilo. Katika somo hili, kwa kutumia ujenzi wa mabwawa makubwa duniani kote kama kifani, wanafunzi watafanya hivyo kupewa taarifa kutokana na mitazamo ya wadau mbalimbali, na kupitia majadiliano ili wajifunze kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali.

**Malengo ya Kufundishia**: Wanafunzi watafanya mazoezi ya kutengeneza hoja zenye msingi wa ushahidi na kuelewa kwamba tofauti za kimaoni mara nyingi hutokana na tofauti za mitazamo ya wadau mbalimbali.

**Kuelewa Malengo**:

- Wanafunzi wataelewa kuwa mitazamo tofauti ya washikadau huzaa maoni tofauti na hitimisho la kimantiki.
- Wanafunzi pia watapata usikivu wa kutambua na kuzingatia sauti zinazokosekana katika majadiliano**.**

**Maswali Muhimu:**

- Je, maoni ya yanawasiliishwa katika kifungu cha taarifa unayasoma? Maoni ya nani yanapaswa kubeba uzito zaidi, na ni nani anayeweza kuamua hilo?
- Hoja kutoka kwa wadau mbalimbali ni tofauti, lakini je, zote zina mantiki na zinaungwa mkono vizuri?
- Sauti za nani hazisikiki?
- Je, tuzingatie vipi masilahi ya viumbe wasio binadamu? Tunapaswa kufikiria jinsi gani mapendezi ya viumbe wasio binadamu?
- Je tutapaswa kuhakikishaje kwamba sauti zaidi zinasikika?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- Toa angalau hoja mbili na ushahidi wake sambamba kutoka katika kifungu cha habari.
- Taja kwa usahihi washikadau wakuu ambao maoni yao yanawasilishwa katika kifungu cha habari.
- Taja angalau mdau mmoja ambaye maslahi yake yamewasilishwa kwa kiasi katika taarifa.
- Taja angalau mdau mmoja ambaye maslahi au mtazamo wake haupo kwenye habari.

**Tathmini:**

- Ubora wa hoja zilizotolewa
- Ushahidi uliotumika kuunga mkono hoja
- Idadi na aina ya washikadau waliotambuliwa kutoka kwenye kifungu cha habari.
- Idadi wa wadau ambao sauti zao hazikuwasilishwa ambazo zilitambuliwa na wanafunzi katika sehemu ya mwisho ya shughuli.

**Mlolongo wa Shughuli:**

- **Maandalizi ya mwalimu**: Kabla ya somo, mwalimu atachagua ujenzi wa bwawa kama mada ya majadiliano kwa darasa. Mwalimu atakusanya pakiti mbili za habari; Taarifa Kifungu A inazingatia uhalali wa serikali wa kujenga bwawa na matatizo ambayo inalenga kutatua, na Kifungu cha Habari B kinazingatia mtazamo wa wenyeji ambao wataathiriwa na kuhamishwa katika eneo la ujenzi wa mabwawa.

- **Sehemu ya 1 (Dakika 5):** Mwanzoni mwa somo, mwalimu atawaelekeza wanafunzi wajigawanye katika vikundi vidogo vya idadi ya 3 hadi 4. Mwalimu ataeleza kuwa somo ni la kujenga uwezo wa wanafunzi kuunga mkono hoja zao kwa ushahidi, na kwamba hapo awali nchi ilikuwa na mipango wa kujenga bwawa lakini kiongozi mpya wa serikali anachukua madaraka na anataka kufanya hivyo kutathmini upya mradi wa bwawa. Kazi ya vikundi vya wanafunzi ni kuishauri serikali na kiongozi mpya juu ya hatua stahiki za kufuata.

- **Sehemu ya 2 (dakika 2):** Nusu ya vikundi vitapokea Kifurushi cha Taarifa A, huku kingine nusu watapata Taarifa katika Kifungu B. Wanafunzi hawatataarifiwa kwamba kuna aina mbili za habari.

- **Sehemu ya 3 (Dakika 13):** Wanafunzi, katika vikundi vidogo, waje na hoja tatu kwa ajili ya ushauri kwa kiongozi mpya wa serikali, na kuunga mkono hoja kwa ushahidi au maoni yanayopatikana kwenye kifungu cha habari.

- **Sehemu ya 4 (dakika 15):** Vikundi vya wanafunzi kuwasilishe hoja na ushahidi wao kwa wanafunzi katika darasa zima.

- **Sehemu ya 5 (Dakika 5):** Mwalimu atajadili na darasa tofauti kuu za ushauri uliotolewa na vikundi tofauti vya wanafunzi. Mwalimu atawabainishia wanafunzi tofauti hiyo kwamba vikundi vimepewa vifungu vya habari kutokana na mitazamo tofauti ya wadau.

- **Sehemu ya 6 (dakika 10):** Vikundi vya wanafunzi viungane na kuunda vikundi vikubwa ili kila kikundi kipya kiwe kina wanafunzi wote wanaosoma Taarifa Pakiti A na wanafunzi wanaosoma Habari Pakiti B. Wanafunzi watajadiliana ili kubaini wadau ambao mitazamo yao na maslahi yanawasilishwa katika kila pakiti ya taarifa kwa kushirikisha darasa zima.

- **Sehemu ya 7 (Dakika 10):** Kisha wanafunzi wajadiliane katika vikundi vidogo au kwa darasa zima wadau ambao mitazamo yao kamili inaweza kuwa haijawasilishwa katika pakiti za habari. Pia wajadili ni mtazamo wa nani wanaoutambua kuwa ni wa kibinafsi zaidi na, ni kwanini.

**Zana kwa/ za a Wanafunzi:**

- Ramani za ‘Google’ na ‘Google Earth’ ili kukagua mabwawa

**Zana za/kwa Walimu:**

- Mabwawa nchini Uchina Three Gorges: https://archive.internationalrivers.org/the-river-educator%E2%80%99s-toolkit-list-of-resources#ThreeGorges
- Zana ya Waelimishaji wa Mto: https://archive.internationalrivers.org/the-river-educator%E2%80%99s-toolkit
- Uchina ya Kisasa, Mjadala wa Bwawa: https://uosm2018.wordpress.com/2014/03/09/the-three-gorges-dam-debate/
- Bwawa la Three Gorges, Janga?: https://www.scientificamerican.com/article/chinas-three-gorges-dam-disaster/
- Mito ya Kimataifa, Gibe III: https://archive.internationalrivers.org/campaigns/gibe-iii-dam-ethiopia
- Bwawa la Belo Monte la Brazili: https://archive.internationalrivers.org/campaigns/belo-monte-dam

**Darasa la 10 Somo la 4**
"Dunia yetu"

**Muda wa muafaka:** dakika 60
**Masomo:** Somo la Jamii
**Viwango: Malengo ya Maendeleo Endelevu yote (**SDGs)
**Imeandaliwa na:** Eva Flavia Martinez Orbegozo

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, wanafunzi kuhusianisha matatizo ya mazingira yao kutambuliwa na ambayo wameyafanyia kazi katika masomo yaliyopita kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

**Lengo la Somo**: Wanafunzi wataelewa jinsi masuala ya kimataifa yanavyounganishwa na ya ndani katika matatizo na kutafakari jinsi maslahi na ujuzi wao unavyoweza kutoa ufumbuzi.

**Malengo**:
- Masuala ya ndani yanaweza kuwa dhihirisho na matatizo ya kimataifa.
- Suluhu za ndani zinaweza kuwa na athari kubwa.
- Watu binafsi wanaweza kuchukua jukumu katika kuboresha ulimwengu kwa kufahamu matatizo ya kimataifa, kujua jinsi yanavyoakisiwa katika muktadha wa eneo lao, na kuhusika katika kutafuta ufumbuzi.

**Maswali Muhimu**:
- Je, matatizo ambayo wanafunzi walikuwa wakiyafanyia kazi yanahusiana vipi na kutofautiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ?
- Ni masuluhisho gani yaliyochunguzwa kupitia mahojiano na utafiti wa jumuiya yanawezekana kuunganishwa katika miktadha mingine?
- Ni lipi linaweza kuonekana kama suluhisho la kimataifa?
- Je, ni sababu zipi zinazowafanya wafanye kazi?
- Ni matatizo gani yanaweza kutokea katika miktadha mingine?
- Ni jinsi gani kuelewa tatizo ambalo wanafunzi wamelifanyia kazi hubadilika wakati wa kujifunza kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ?

**Malengo ya Ujifunzaji kwa Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- Kuunganisha matatizo ya ndani na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa kuunganisha matatizo yao na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ambayo yanahusiana, na kuonyesha uhusiano.
- Zungukia kati ya miktadha ya ndani na ya kimataifa kwa kutathmini uwezekano wa uhalali wa suluhu walizokutana nazo katika vikao vilivyotangulia katika miktadha mingine duniani.
- Kuwasilisha uhusiano kati ya ndani na (nje) kimataifa, na matatizo yanayoweza kutokea wakati wa kutafsiri suluhu kati ya miktadha.

**Tathmini:** Matangazo ya habari yameandikwa na kupitishwa katika vikundi (na ikiwezekana, kurekodiwa)

**Mlolongo wa Shughuli**:

**Sehemu ya 1 (Hisia)**: Ujanibishaji

- Mfano wa suluhisho la ndani lililofanikiwa:
    - Wanafunzi kuonyeshwa video kuhusu kutumia chupa za plastiki zilizojazwa maji na kutobolewa ili ziwe na mwangaza ndani ya nyumba bila mwanga wa asili au umeme.
    - Unganisha kwa picha mjongeo (video): https://www.youtube.com/watch?v=cQCHvO2H0_0
    - Kama hakuna uwezekano wa kuonyesha picha mjongeo (video), hadithi inaweza kusimuliwa na picha chache zinaweza kuonyeshwa.
- Majadiliano na Tafakuri: Mwalimu awaambie wanafunzi kuzingatia maswali yafuatayo (kwanza katika jozi na kisha katika majadiliano ya kikundi kizima):
    - Je, ni matatizo gani tofauti tofauti ambayo suluhisho hili linajaribu kushughulikia (kama vile ukosefu wa umeme)?
    - Je, ni sababu zipi kubwa za matatizo hayo (kama vile umaskini)?
    - Mwalimu anaweza kuandika matatizo na visababishi vinavyo husiana na SDGs (kama vile umaskini, nishati nafuu na usafi, miji endelevu, n.k.).

**Sehemu ya 2 (tafakari):** Mwalimu anapaswa kutambulisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), kwa kuzingatia muktadha.

- Wanafunzi wanaulizwa wafikirie kuhusu matatizo ambayo wamesikia na kutambua matatizo yanayohusiana na jumuiya yao na kikao kilichopita.

    - Wanafunzi hujibu swali lifuatalo: Tatizo lako limeunganishwa kivipi na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ? Tambua Malengo yote ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ambayo shida zako zimehusiana nayo.
- Mwalimu ataweka karatasi zenye majina la kila Lengo la Maendeleo Endelevu (SDG) kwenye kuta darasani. Wanafunzi watakuwa na kadi ndogo au kuziweka na jina la tatizo, na wanahitaji kuamua ni Malengo (SDGs) gani wanaweza kuweka na tatizo lao.
- Wanafunzi huzunguka darasani na kuchapisha tatizo lao chini ya Malengo (SDGs) mengi nyingi kadiri inavyowezekana. Dakika mbili za mwisho za shughuli hili zitatumika kwa mwalimu kuwambia wanafunzi wachache kuhalalisha na kueleza jinsi tatizo lao linavyohusiana na Malengo (SDGs) waliyoyachagua.
- Mwalimu anaweza kuwawezesha wanafunzi kujadili maswali yafuatayo katika jozi:
    - Ulichagua tatizo gani?
    - Je, unaweza kueleza tatizo?
    - Nani anaathiriwa na tatizo hilo?
    - Tunajuaje?
    - Ni Malengo (SDGs) yapi yanayoweza kushughulikia tatizo hilo?
    - Je, wanalishughulikiaje?

**Sehemu ya 3 (Tenda):** Matangazo ya habari kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na tatizo la karibu nawe:

- Matayarisho: Wanafunzi wataombwa kuandika tangazo la habari ambalo linajumuisha maswali yafuatayo:
    - Umechagua tatizo gani?
    - Je, unaweza kueleza tatizo?
    - Nani anaathiriwa na tatizo hilo?
    - Tunajuaje?
    - Ni Malengo (SDGs) yanayoweza kushughulikia tatizo hilo?
    - Wanalishughulikiaje?
- Wanafunzi wanatakiwa kuandika maandishi kana kwamba wanaripoti kwa kituo cha habari cha jamii (yaani, wanafunzi wanatakiwa kuangazia habari hii, tatizo, na wito wa kuchukua hatua kutatua tatizo hilo).
- Sehemu ya 3 inapaswa kujumuisha rekodi ya matangazo (kama inawezekana) na kuchezwa kwa ajili ya darasa ama wanafunzi wanaweza tu kuidhinisha mbele ya darasa.

**Zana za  Wanafunzi**:

- Tovuti ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) (au machapisho yenye SDGs zilizoorodheshwa)
    - https://sdgs.un.org/goals
- Maelezo ya darasa kutoka katika masomo yaliyotangulia
- Mambo yanayoweza kutolewa kutoka katika masomo yaliyotangulia

**Zana za/kwa Walimu**:

- Tovuti ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).
    - https://sdgs.un.org/goals

**Darasa la 10 Somo la 5**
**"Mradi wa msingi" (Kazi Mradi)**

**Muda Mwafaka:** Dakika 60 kwa kila somo
**Somo**: Uandishi wa Ubunifu, Somo la Kijamii
**Viwango**: Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yote
**Imeandikwa na:** Madhuri Dhariwal

**Muhtasari na Mantiki**: Wanafunzi wataweka pamoja utafiti ambao wamefanya katika masomo ya awali ili kutoa nakala moja, kwa lengo la kuchapisha.

**Kuelewa Malengo**:
- Ulimwengu umeunganishwa.
- Vitendo vidogo vinaweza kuwa na athari kubwa.
- Kufanya utafiti ni muhimu na kunahusisha mchakato.

**Maswali Muhimu**:
- Je, tunaunganisha vipi vipande mbalimbali vya utafiti?
- Nini jukumu langu katika kutatua matatizo duniani?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**
- Kuelewa uhusiano kati ya maadili wanayoshikilia na matatizo wanayotambua katika mazingira yao.
- Kuangaliangalia kama matatizo wanayofikiri yapo katika jamii yao.
- Kuandikandika karatasi zenye urefu tofauti kwa kila somo.
- Kukusanya maandishi yao katika kipande kimoja chenye kushikamana.
- Kuhaririariri kazi zao wenyewe.
- Kujengaenga muungano/Umoja kati yao wenyewe, mazingira yao ya karibu, ulimwengu kwa ujumla, na jukumu lao katika kutatua matatizo ya ulimwengu.

**Tathmini:** Wanafunzi watawasilisha mradi wa mwisho uliofanyiwa utafiti vizuri, ulioelezewa vizuri ambao huonyesha changamoto mbalimbali za kimataifa na mapendekezo yanayoweza kutumika kutatua. Mwalimu ataweka alama kwa hiari yake.

**Mlolongo wa Shughuli:**

**Utangulizi (Dakika 5):** wanafunzi kuandika (nakala) moja, wakijenga hoja juu ya kazi walizozifanya katika masomo yaliyopita.

**Majadiliano Kuhusu Mfumo wa Karatasi (Dakika 10)**: Toa muhtasari wa mfumo wa karatasi:

- Utangulizi na taarifa ya tatizo
- Mbinu (kukagua mbinu tofauti: mahojiano, vyanzo vya pili, dhana kuu zilizojadiliwa, nk.)
- Umuhimu wa tatizo (Unajuaje kuwa ni tatizo? Kwa nini ni tatizo? Nini kifanyike?)
- Mawazo makuu yaliyotolewa kutokana na mahojiano
- Utafiti juu ya ukengeufu chanya
- Uhusiano na tatizo la ulimwengu
- Suluhisho linalopendekezwa
- Marejeleo
- Viambatanisho
- Mbadala: Utafiti unaweza kuwasilishwa katika muundo wowote bunifu wa mwandishi - hadithi, ubao wa picha, mashairi n.k.

**Kuanza Kukusanya (Dakika 30):** Katika vikundi vyao, wanafunzi wataanza kuweka pamoja kazi waliyoifanya. Kisha watagawana kazi kati yao wenyewe na kuwa na rasimu ifikapo mwisho wa darasa.

**Wasilisho (Dakika 10):** Kila kikundi kitakuwa na dakika 1-2 kuwasilisha kwa darasa zima taarifa ya tatizo na suluhisho lao lililopendekezwa.

**Hatua Zinazofuata (Dakika 5):** Wanafunzi wataombwa kuboresha kazi zao nyumbani na kuwasilisha rasimu ndani ya wiki ijayo. Mwalimu atakagua rasimu, atazirudisha pamoja na maoni, na wanafunzi watarekebisha na kuwasilisha. Kisha mwalimu anaweza kuziunganisha na kuwasilisha kwa Mkuu au kujaribu yeye mwenyewe kupata nakala zilizochapishwa kama kitabu cha pamoja. Wanafunzi pia wanaweza kuhusika katika mchakato huu.